


TUME YA VYUO VIKUU TANZANIA (TCU)



TAARIFA KWA UMMA

WAOMBAJI WALIODAHILIWA ZAIDI YA CHUO KIMOJA KATIKA AWAMU YA TATU YA UDAHILI MWAKA WA MASOMO 2019/2020

Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) inatangaza kuwa udahili kwa awamu ya tatu katika Taasisi za Elimu ya Juu kwa mwaka wa masomo 2019/2020 umekamilika. Majina ya waombaji waliodahiliwa katika awamu ya tatu yameshatangazwa na vyuo husika.

Waombaji waliodahiliwa chuo zaidi ya kimoja katika awamu ya tatu na wale wa awamu zilizopita ambao bado hawajathibitisha udahili wao katika chuo kimoja, wanasisitizwa kuthibitisha udahili wao katika chuo kimoja kuanzia tarehe 21 hadi 30 Septemba, 2019. Jinsi ya kujithibitisha ni kwa kutumia ujumbe mfupi wenye namba maalum ya siri uliotumwa kupitia namba za simu au barua pepe walizotumia wakati wa kuomba udahili. Wale ambao hawatapata kwa wakati ujumbe huo wanashauriwa kuingia kwenye mifumo ya udahili ya vyuo walivyodahiliwa na kuomba kutumiwa ujumbe mfupi wenye namba maalum ya siri ili kujithibitisha.

Tume **inasisitiza** kuwa, uthibitisho wa udahili ufanyike kupitia akaunti waombaji walizotumia wakati wa kuomba udahili katika vyuo walivyodahiliwa. Orodha ya majina ya waombaji waliodahiliwa zaidi ya chuo kimoja katika awamu ya tatu na awamu zilizopita ambao hawajathibitisha udahili imewekwa kwenye tovuti ya TCU (www.tcu.go.tz).

Aidha, waombaji wote wanakumbushwa kuwa masuala yote yanayohusiana na udahili ama kujithibitisha yawasilishwe moja kwa moja kwenye vyuo husika na siyo TCU.

Imetolewa na:



Prof. Charles D. Kihampa

Katibu Mtendaji

Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania

20 Septemba, 2019